JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI



TAARIFA YA MAFANIKIO YA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI KATIKA KUTEKELEZA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2005 KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU (DESEMBA 2005 - DESEMBA 2008)

DESEMBA 2008

1. UTANGULIZI

Wizara ya Fedha na Uchumi inaongozwa na Waziri akisaidiwa na Naibu Mawaziri Wawili. Aidha, Wizara ina Katibu Mkuu ambaye pia ni Mlipaji Mkuu wa Serikali na anasaidiwa na Naibu Makatibu Wakuu Watatu. Wizara hii ina Idara na Taasisi zinazojitegemea ikiwa ni pamoja na Benki Kuu, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Takwimu ya Taifa, Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma n.k.

2. DIRA NA DHIMA YA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

Wizara ya Fedha na Uchumi imejipanga kutoa huduma kwa ufanisi wa hali ya juu ili kuongoza juhudi za Serikali za kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Ili kutekeleza hayo, Wizara ya Fedha na Uchumi imejiwekea **Dira** ya kuwa taasisi inayoongoza jitihada za kuwa na ukuaji uchumi ambao ni endelevu na unaozingatia usimamizi bora wa rasilimali fedha za Umma. Aidha, **Dhima** ya Wizara ni kuhakikisha kuwepo na uchumi endelevu kwa kubuni sera sahihi za fedha na za kibajeti na kukuza dhana ya matumizi ya mtandao wa kompyuta katika uchumi.

3. MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI

Ili kufanikisha Dhima na Dira kama ilivyoelezwa hapo juu, majukumu ya Wizara ya Fedha na Uchumi ni pamoja na kuchambua na kubuni sera za uchumi jumla; kuweka mazingira bora ili kuwezesha sekta binafsi kushamiri na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii; kuibua na kubainisha fursa za kuvutia uwekezaji; kuandaa na kusimamia sera za mapato na matumizi ya serikali; kuandaa na kusimamia sera za madeni na mkakati wa kuyadhibiti; kuandaa na kusimamia sera za fedha na urari wa malipo na nchi za nje;

kusimamia takwimu zote zinazohusu uchumi na sekta ya fedha; kuratibu utekelezaji wa MKUKUTA; kusimamia matumizi ya fedha za umma na kudhibiti fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya kigaidi.

4. ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2005

Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na taasisi zilizo chini yake inaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 kama ilivyoanishwa katika chapisho lake la Agosti 2005. Aidha, katika kutekeleza hayo, Wizara imeongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA) na Sera za Fedha na maelekezo mengine ya Serikali. Kulingana na Ilani hiyo, Wizara inatakiwa kujikita katika maeneo ya kusimamia uchumi jumla; kusimamia bajeti ya serikali; kuzipatia rasilimali fedha sekta za kijamii, uzalishaji, mawasiliano na miundombinu; kuboresha sekta ya fedha katika maeneo ya usimamizi, uwezeshaji upatikanaji wa mikopo na kuwawezesha wajasiriamali; kuboresha huduma kwa wastaafu na kuimarisha mashirika ya umma/ubinafsishaji.

5. MAFANIKIO YA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI KATIKA KUTEKELEZA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2005

Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na taasisi zake katika kipindi cha Desemba 2005 hadi Desemba, 2008 imefanikisha mengi katika ahadi mbalimbali zilizotolewa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kama ifuatavyo:-

5.1 USIMAMIZI WA UCHUMI JUMLA

Katika usimamizi wa Uchumi Jumla, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 imebainisha malengo yafuatayo:

(i) Kukuza uchumi kwa kiwango cha asilimia kumi (10%) kwa mwaka ifikapo 2010 kutoka ukuaji wa mwaka 2005 wa asilimia 6.7

(ii) Kujenga msingi wa uchumi wa kisasa, wa Taifa linalojitegemea.

Utekelezaji

Katika kipindi cha miaka mitatu (2006 - 2008) uchumi umekua kwa wastani wa asilimia 7.1, mwenendo ambao ni wa kuridhisha ikizingatiwa kuwepo kwa mtikisiko wa kiuchumi duniani pamoja na hali mbaya ya hewa iliyoathiri uzalishaji katika sekta za kilimo na viwanda katika miaka ya karibuni.


Mwenendo wa mfumuko wa bei ukiacha kipindi hiki cha robo ya nne ya mwaka 2008 ambapo kiwango kilipanda sana, kwa ujumla umeonyesha mwenendo wa kuridhisha tokea mwaka 2005 hadi katikati ya mwaka 2008.

Ili kujenga Uchumi wa kisasa, wa Taifa linalojitegemea, tunahitaji kuboresha sekta zote za uchumi na maendeleo ya jamii. Tunahitaji kilimo cha kisasa, chenye tija kubwa na ufanisi. Haya yanawezekana kama rasilimali fedha zitaelekezwa katika kupata pembejeo za kutosha hasa mbolea, mbegu bora na madawa ya wadudu, kupanua

kilimo cha umwagiliaji na uhakika wa upatikanaji masoko. Aidha, tunahitaji vilevile kuwa na viwanda vya kisasa na teknolojia bora ili kuzalisha bidhaa za viwandani zilizo bora na zinazohimili ushindani. Tunahitaji kuwa na miundombinu imara hasa barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege ili kurahisisha usafiri na usafirishaji. Kadhalika tunahitaji kuimarisha sekta za maendeleo ya jamii ili kuboresha rasilimali watu.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Nne, Wizara ya Fedha na Uchumi imeelekeza rasilimali fedha kwa kiwango kikubwa katika maeneo hayo. Mgawanyo wa rasilimali fedha katika maeneo ya kilimo, miundombinu, elimu, afya na maji kwa kipindi cha miaka mitatu 2005 hadi 2008 ni kama inavyoonyeshwa kwenye *kielelezo Na.1*

Kielelezo Na. 1: Mgao wa rasilimali kwa maeneo ya kipaumbele kwa kipindi 2005/6 - 2007/8



5.2 USIMAMIZI WA BAJETI YA SERIKALI

Kama ilivyoelezwa hapo awali, Wizara ya Fedha na Uchumi ina jukumu la kusimamia Bajeti ya Serikali ikiwa ni pamoja na mapato, matumizi na mikopo ya kujazia pengo kati ya mapato na matumizi. Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Nne, bajeti ya Serikali imekuwa ikiongezeka na hivyo kuwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya uendeshaji na utekelezaji miradi. Bajeti ya Serikali imeongezeka kutoka shilingi trilioni 4.18 mwaka 2005/06 hadi shilingi trilioni 7.22 katika mwaka 2008/09 sawa na ongezeko la asilimia 72.8

5.2.1 Mapato ya ndani

Mapato ya ndani ya Serikali yanatokana na mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Mapato ya kodi yanajumuisha kodi ya mapato, ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa, wakati mapato yasiyo ya kodi yanajumuisha ada za leseni, mapato ya gawio la Serikali, kodi za viwanja nk. Ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Serikali umeongezeka kutoka shilingi bilioni 1,951.3 mwaka 2005 hadi shilingi bilioni 4,133.2 mwaka 2008. Kiwango hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 111.8.

Mapato ya Kodi

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya awamu ya nne, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeweza kupata mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa mapato. Mapato yanayokusanywa na TRA yameongezeka kutoka shilingi bilioni 1,757.4 mwaka 2005 hadi shilingi bilioni 3,802.2 mwaka 2008.

Kiwango hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 116.4 *(kielelezo Na. 2).* Mamlaka ya Mapato Tanzania inachangia zaidi ya asilimia 90 ya mapato ya ndani ya Serikali Kuu. Mapato ya kodi yameongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na sababu zifuatazo: -

(i) Kuendelea kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji na biashara, kupanuliwa wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya;


(ii) Kuanzishwa kwa kitengo cha walipa kodi wakubwa;

(iii) Kuendelea kurekebishwa kwa mfumo wa kodi;

(iv) Utekelezaji wa mageuzi makubwa ndani ya TRA chini ya Mpango wake wa Pili wa maboresho ambao umekuwa msingi wa kukua kwa mapato mwaka hadi mwaka. Hivi sasa Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanza kutekeleza Mpango wa tatu wa Miaka Mitano wa maboresho 2008/09 hadi 2012/13; na

(v) Ushirikiano mzuri baina ya walipa kodi na wakusanya kodi

Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa mapato ya ndani kwa kipindi cha 2005 - 2008



Mapato yasiyo ya Kodi

Mapato yasiyo ya kodi kwa mwaka 2008 yanakisiwa kufikia shilingi bilioni 284.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 194 mwaka 2005, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 46.5.

5.2.2 Misaada na mikopo ya nje

Kutokana na hatua ambazo Serikali imechukua katika kusimamia uchumi na maendeleo ya jamii, washirika wa maendeleo wameunga mkono juhudi hizo za Serikali kwa kuendelea kuongeza misaada na mikopo. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita jumla ya misaada na mikopo imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 1,712.4 mwaka 2005/06 hadi Shilingi bilioni 2,429.5 mwaka 2008/09 sawa na ongezeko la asilimia 41.8. Serikali imechukua hatua za makusudi za kuelekeza

misaada na mikopo ya wahisani kwa kuwekeza zaidi katika miradi ya maendeleo na kijamii ili baadaye kupunguza utegemezi hatua kwa hatua.

5.2.3 Mwenendo wa Deni la Taifa

Wizara ya Fedha na Uchumi imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Madeni ili kudhibiti ongezeko la Deni la Taifa lisizidi kiwango kinachohimilika. Katika utekelezaji wa Mkakati huo, Serikali imedhibiti ukopaji holela. Aidha, uamuzi wa wahisani wa kusamehe baadhi ya madeni yao, umepunguza mzigo wa malipo ya madeni katika bajeti ya Serikali. Hadi kufikia Desemba, 2007, Deni la Taifa lilifikia dola za Marekani milioni 7,041.3, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 9,383.9 Desemba 2005, ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 25. Kati ya deni hilo dola milioni 5,367.8, sawa na asilimia 76.2 ya deni lote lilikuwa deni la nje na dola milioni 1,673.5, sawa na asilimia 23.8 lilikuwa deni la ndani.

5.2.4 Usimamizi wa matumizi

Moja ya majukumu ya Wizara ya Fedha na Uchumi ni kusimamia matumizi ya fedha za Serikali ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinakasimiwa na kutumika katika maeneo yaliyokusudiwa. Aidha, hatua hii inalenga kupata thamani halisi ya matumizi ya fedha husika.

Wizara ya Fedha na Uchumi imekuwa ikiipatia Ofisi ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali fedha za kutosha kukidhi mahitaji ya ukaguzi. Aidha, Wizara imesimamia utayarishaji na kupitishwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, kwa lengo la kuipa Ofisi ya Ukaguzi, uhuru zaidi katika utekelezaji wa majukumu yake. Hivi sasa

Ofisi ya Taifa ya ukaguzi inatoa taarifa za ukaguzi wa vyombo vyote vya umma kwa wakati. Aidha, Kamati za Bunge za kusimamia matumizi zimeimarishwa ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Ili kupunguza tatizo la wataalam wa uhasibu na ukaguzi, Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kushirikiana na TAMISEMI imewezesha kuajiriwa kwa wahasibu na wakaguzi wa ndani 1,224 na kuwapangia kazi katika Serikali za Mitaa, Mikoa na Wizara. Aidha, Wizara ya Fedha na Uchumi ipo katika hatua za mwisho ya kuajiri zaidi wahasibu na wakaguzi wa ndani wapatao 617 na kuwapangia kazi katika Mikoa na Serikali za Mitaa. Watumishi 937 waliopo kazini katika fani za Uhasibu, Ukaguzi wa ndani, wataalamu wa Ugavi na Manunuzi, na wataalam wa kompyuta pia wamepatiwa mafunzo zaidi ili kuwaongezea ujuzi katika kazi zao.

Mfumo maalum wa kompyuta (IFMS – Intergrated Financial Management System) unaounganisha Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na baadhi ya Halmashauri umewezesha Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kuwasiliana na Idara zote za uhasibu na hivyo kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa mapato na matumizi ya Serikali. Aidha, kuanzia Desemba 2006, Serikali imeweza kulipa mishahara ya watumishi wake kila tarehe 23 ya mwezi, kinyume na siku za nyuma. Hii imesaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza kero za watumishi.

5.3 KUZIPATIA RASILIMALI FEDHA SEKTA MBALI MBALI:

Wizara ya Fedha na Uchumi, imeendelea kutoa rasilimali fedha kwa sekta mbalimbali ili kuweza kutekeleza majukumu yao.

5.3.1 Sekta za Kijamii

Katika kutekeleza malengo ya Ilani ya Uchaguzi, Wizara ya Fedha na Uchumi imeendelea kutenga fedha zaidi katika sekta za jamii kwa lengo la kumwezesha mwananchi kupata huduma muhimu katika sekta za elimu, maji na afya. Katika mwaka 2008/09 sekta hizo zimetengewa kiasi kikubwa cha fedha ikilinganishwa na mwaka 2005/06 kama ifuatavyo:-

(i) Sekta ya afya imetengewa shilingi bilioni 803.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 365.8 mwaka 2005/06.

(ii) Sekta ya elimu imetengewa shilingi bilioni 1,430.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 669.5 mwaka 2005/06.

(iii) Sekta ya maji imetengewa shilingi bilioni 230.6 mwaka 2008/09 ikilinganishwa na shilingi bilioni 159.9 mwaka 2005/06.

5.3.2 Sekta za Uzalishaji

Wizara ya Fedha na Uchumi imeendelea kuzingatia vipaumbele vya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini katika maeneo ya uzalishaji mali ikiwa ni pamoja na kilimo. Katika mwaka wa fedha 2008/09 sekta ya kilimo imetengewa jumla ya shilingi bilioni 460 katika maeneo ya ruzuku ya pembejeo na miradi mingine ya maendeleo katika sekta hiyo. Kiwango hiki cha mgao wa fedha kwa mwaka 2008/09 ni sawa na ongezeko la shilingi bilioni 291.3 ikilinganishwa na 2005/06. Sekta zingine za uzalishaji ikiwemo viwanda, uvuvi na maliasili nazo zimeendelea kupata mgao wa fedha nyingi zaidi kulingana na uwezo wa Serikali.

5.3.3 Sekta ya Mawasiliano na Miundombinu

Wizara ya Fedha na Uchumi imeendelea kutoa rasilimali fedha kwa sekta ya mawasiliano na miundombinu kulingana na uwezo wa Serikali ikiwa ni pamoja na kugharimia ujenzi wa barabara, madaraja, ununuzi wa vivuko. Aidha, upanuzi wa viwanja vya ndege unaendelea.

5.4 KUBORESHA SEKTA YA FEDHA

5.4.1 Usimamizi wa Sekta ya Fedha

Katika usimamizi wa sekta ya fedha, Ilani ya Uchaguzi imeelekeza kufanya yafuatayo:

(i) Kuendelea kuimarishwa kwa sekta ya fedha ili iweze kukabili ipasavyo changamoto ya huduma na kupanuka kwa uchumi wa Taifa.

(ii) Miongoni mwa mambo yatakayoshughulikiwa ni suala la riba za mabenki kwa mtazamo wa kupunguza tofauti kubwa baina ya riba za kukopesha na riba za kukopea.

(iii) Kuweka mazingira mazuri ya kujenga tabia ya kujiwekea akiba miongoni mwa wananchi na kurahisisha upatikanaji wa mikopo

Utekelezaji

Ili kufanikisha hayo, Wizara ya Fedha na Uchumi imechukuwa hatua zifuatazo:

Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kufanya mageuzi katika Sekta ya Fedha ambayo yanalenga zaidi kurekebisha Sera na Sheria mbalimbali za fedha ili kuiwezesha sekta binafsi kuchangia kikamilifu katika kukuza uchumi na kuongeza Pato la Taifa. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania imeanza kutekeleza Programu ya Awamu ya Pili ya Kurekebisha Sekta ya Fedha (Second Generation Financial Sector Reform Program 2006 – 2010) ambapo mambo yafuatayo yametekelezwa:

(i) Kutungwa kwa Sheria mpya ya Benki Kuu ya mwaka 2006 na Sheria ya mabenki na vyombo vya fedha ya mwaka 2006 kwa lengo la kuongeza ufanisi wa Benki Kuu katika kusimamia sekta ya fedha.

(ii) Kutungwa kwa Sheria inayoweka mazingira ya kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa njia ya ukodishaji vifaa, mitambo na rasilimali nyingine (lease financing).

(iii) Wizara imefanya mchakato wa uanzishaji wa mikopo ya nyumba (mortgage financing) na umefikia katika hatua za mwisho. Utaratibu huu utawezesha upatikanaji wa mikopo ya nyumba kwa wananchi walio wengi.

(iv) Serikali imechukua hatua za kuiimarisha Benki ya Rasilimali (TIB) kwa kuanza kuiongezea mtaji ili iweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Kwa kuanzia, Serikali imeruhusu kiasi cha shilingi bilioni 17.5 za Mradi wa Ukarabati wa Sekta ya Mafuta ya Petroli zilizokuwa zikisimamiwa na TIB

kwa niaba ya Serikali zitumike kama mtaji wa TIB. Aidha, Wizara ya Fedha na Uchumi katika Bajeti yake ya mwaka 2008/09 imetenga kiasi cha shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kuongeza mtaji wa TIB.

(v) Serikali imeandaa na kupitisha Sheria ya kusimamia mifuko ya Hifadhi za Jamii ili kusimamia sekta hii. Pia, Sheria hiyo, inatoa nafasi ya kuanzishwa kwa msimamizi (Regulator) wa mifuko hiyo ili kuhakikisha pamoja na mambo mengine uzingatiaji wa miongozo ya uwekezaji (standard investment guidelines).

5.4.2 Kuwezesha Upatikanaji wa Mikopo

Mikopo iliyotolewa kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi iliongezeka kutoka shilingi bilioni 1,656.8 mwaka 2005/06 hadi shilingi bilioni 2,260 mwaka 2006/07, sawa na ongezeko la asilimia 36.4. Mikopo katika sekta binafsi iliongezeka kutoka shilingi bilioni 2,028.3 Desemba, 2006 hadi shilingi bilioni 2,883.8 Desemba 2007. Mikopo mingi ilielekezwa katika shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani, biashara, kilimo, usafirishaji kwa na mawasiliano.

Shughuli mbalimbali za kiuchumi zilizopata viwango vikubwa vya mikopo ni: bidhaa za viwandani (asilimia 19.3), biashara (asilimia 17.2); mikopo binafsi (asilimia 16.2). Kuongezeka kwa mikopo iliyotolewa kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi kulitokana na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara, kuongezeka wateja na kuongezeka kwa ushindani baina ya benki zinazotoa mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, mwenendo huu umechangiwa na uamuzi wa

Serikali kuendelea kutekeleza sera ya kutokukopa kutoka benki za biashara ili benki hizo ziweze kukopesha zaidi sekta binafsi.

5.4.3 Kuwawezesha wajasiriamali

Katika eneo hili, Ilani ya Uchaguzi imeelekeza yafuatayo:

(i) Kuwa na mipango ya kuwapa fursa wajasiriamali Watanzania wanaoinukia kupata uzoefu wa wajasiriamali wa nchi nyingine za kusini.

(ii) Kuelekeza nguvu katika kuwawezesha wananchi, hasa vijana na wanawake, kwenye shughuli za kujiajiri vijijini na mijini.

(iii) Kuandaa mipango ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwenye kila wilaya.

(iv) Kupanua wigo wa harakati za kiuchumi zinazozalisha ajira nyingi ili kuongeza fursa kwa vijana.

(v) Kupanua na kuimarisha fursa ya ushiriki wa walemavu katika siasa na uendeshaji wa uchumi .

Utekelezaji

Katika kufanikisha utekelezaji wa maelekezo haya, Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kushirikiana na Benki Kuu imetekeleza yafuatayo:

Mifuko ya dhamana ya mikopo (Credit Guarantee Scheme)

Kuanzishwa kwa Mfuko wa Dhamana wa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati (SME Credit Guarantee Scheme) ambao unaratibiwa na Benki Kuu kumeboresha mazingira ya wenye mitaji midogo na ya kati waweze kupata mikopo kutoka kwenye mabenki na taasisi za fedha. Tangu mfuko huu uanzishwe, jumla ya SMEs 48 zimepata udhamini wa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 2,970.67. Aidha, mikopo hii ilielekezwa katika maeneo ya kiuchumi yafuatayo: Uzalishaji wa chakula, Ujenzi, Shughuli za hoteli na Utalii, Sekta ya Elimu, Afya na maji, mawasiliano usafirishaji na Ufugaji wa kuku na Uvuvi.

Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi wa wajasiriamali wadogo (Mfuko wa JK)

Kuanzishwa kwa Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi kwa ajili ya wajasiriamali wadogo kumesaidia vikundi mbalimbali kupata mikopo nafuu. Hadi tarehe 30 Septemba, 2008, Serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi wa JK- awamu ya kwanza ilikopesha kiasi cha Shilingi bilioni 39.0 kupitia benki ya NMB (Shilingi bilioni 16.3) na CRDB (Shilingi bilioni 22.7). Hii ni asilimia 124 ya Shilingi bilioni 31.5 zilizotarajiwa kutolewa na benki hizo mbili. Jumla ya wajasiriamali 48,339 wamefaidika na mikopo iliyotolewa. Kati yao wajasiriamali 26,384 na 21,955 walikopeshwa kupitia benki ya CRDB na NMB kwa mtiririko huo.

Katika awamu ya pili, Serikali imetoa Shilingi bilioni 10.5; kati ya hizo Shilingi milioni 600 zilipelekwa Zanzibar na Shilingi bilioni 9.9 Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Bara Serikali ilizigawa

fedha hizi kwa Taasisi za fedha 14 kupitia makundi mawili. Kundi la kwanza ni la Benki na Taasisi za fedha ambazo zina mitaji midogo na zinakopesha fedha hizi moja kwa moja kwa wananchi chini ya mfumo wa “Revolving Fund” na kundi la pili ni la Benki zinazoshiriki katika mfumo wa dhamana ambapo zinakopesha mara tatu ya fedha walizopewa chini ya mfumo wa “Revolving Fund”. Benki hizo ni pamoja na Tanzania Postal Bank, CRDB Bank na Akiba Commercial Bank; Taasisi nyingi zilizobaki ziko kwenye kundi la kwanza.

Hadi kufikia Septemba, 2008 mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 4.198 ilitolewa na benki na asasi ndogo za fedha kwa wajasiriamali wadogo kwa mchanganuo unaoonyeshwa kwenye jedwali na. 3:

Jedwali Na. 1: Mikopo iliyotolewa na Benki na Asasi ndogo za Fedha katika Awamu ya Pili ya Mfuko wa Uwezeshaji

CRDB Bank	1,440,967,300
Akiba Commercial Bank	70,000,000
Kagera Farmers Coop. Bank	220,684,000
Kilimanjaro Coop. Bank	174,490,000
Uchumi Commercial Bank	77,469,000
Mwanga Community Bank	92,150,000
Pride Tanzania	100,000,000
Presidential Trust Fund	110,837,000
SCCULT	1,409,697,650
DUNDULIZA	56,480,000
Tanzania Postal Bank	245,967,000
Azania Bank	200,000,000
Jumla	**4,198,741,950**

5.5 KUBORESHA HUDUMA KWA WASTAAFU

Ilani ya Uchaguzi inaelekeza Wizara kuhakikisha kuwa wazee wanaostaafu katika utumishi wa Serikali na Taasisi zake wanalipwa mafao yao bila usumbufu wowote.

Utekelezaji

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya awamu ya nne, juhudi mbalimbali za kuboresha huduma kwa wastaafu zimefanyika kwa lengo la kuwaondolea kero wastaafu kwa kuwalipa mafao yao bila usumbufu. Mafanikio ambayo tayari yamepatikana ni pamoja na:

(i) Kuhamishia huduma ya kuwalipa wastaafu kwenye Mifuko ya Hifadhi za Jamii kwa sababu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wanao utaalamu na uzoefu wa kutoa huduma kwa wastaafu. Wastaafu ambao wapo kwenye daftari la pensheni la Hazina ambao ni 53,600 wamehamishiwa katika Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) ambao wameanza kulipwa Pensheni zao kuanzia Julai, 2008. Wastaafu wengine ambao ni askari Polisi na Magereza wamehamishiwa kwenye Mfuko wa GEPF tangu Januari 2008. Aidha, viongozi wengine wa kitaifa waliostaafu wanaendelea kulipwa mafao yao Hazina.

(ii) Kuwaondolea usumbufu wastaafu waliokuwa na ajira mbili ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa kulipwa mafao yao katika kituo kimoja badala ya kulipwa katika vituo viwili tofauti.

(iii) Wastaafu walioko kwenye daftari la Hazina wanalipwa pensheni zao kupitia akaunti binafsi badala ya utaratibu wa kulipiwa

kwenye kaunta za benki. Utaratibu wa kila Mstaafu kuwa na akaunti yake binafsi umewezesha kila Mstaafu kupewa kadi ya huduma ya kuchukulia fedha (ATM), ambapo mstaafu anaweza kuchukua fedha yake mahali popote penye huduma hiyo na kwa wakati wowote anapohitaji.

(iv) Kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za wastaafu walioko kwenye daftari la Hazina kwa kuweka kumbukumbu zao kwenye mfumo wa kompyuta ili kuwaondolea usumbufu wanapofika kufuatilia madai yao.

(v) Yamefanyika mafunzo ya kikanda yaliyowahusisha waajiri, hasa maafisa wanaoshughulikia mafao na mirathi katika Wizara na Mikoa kuhusu wajibu wao wa kushughulikia mafao ya kustaafu na mirathi. Mafunzo haya yamefanyika kama ifuatavyo:

- Kanda ya Ziwa iliyohusisha Mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara na Shinyanga ilifanyika jijini Mwanza kuanzia tarehe 20/11/2008 hadi tarehe 21/11/2008.

- Kanda ya Kaskazini iliyohusisha Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, na Tanga, mafunzo yalifanyika kuanzia tarehe 24/11/2008 hadi 25/11/2008 mjini Arusha.

- Kanda ya kati iliyohusisha mikoa ya Dodoma, Kigoma, Tabora, na Singida, mafunzo yalifanyika kuanzia tarehe 28/11/2008 hadi 29/11/2008 mjini Dodoma.

- Kanda ya kusini iliyohusisha mikoa ya Lindi, Morogoro, Mtwara, na Pwani, mafunzo yalifanyika kuanzia tarehe 01/12/2008 hadi tarehe 02/12/2008, mjini Morogoro.

- Kanda ya nyanda za juu iliyohusisha mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa,na Ruvuma, mafunzo yalifanyika kuanzia tarehe 05/12/2008 hadi tarehe 06/12/2008 jijini Mbeya.

- Mafunzo kwa mkoa wa Dar es Salaam yalifanyika kuanzia tarehe 12/12/2008 hadi 13/12/2008 jijini Dar es Salaam.

(vi) Hadi Juni, 2008, wastaafu 21,152 waliokuwa wamelipwa pensheni zao kwa mkupuo na kuondolewa kwenye daftari la wastaafu, wamerejeshwa kwenye daftari kufuatia uamuzi wa Serikali wa mwaka 2004/2005 wa kuwarejesha kwenye daftari wastaafu wote waliokuwa wamelipwa pensheni zao kwa mkupuo.

Aidha, elimu kwa umma ilitekelezwa kupitia vyombo vya habari, kama vile TBC Taifa, Radio Tumaini na Radio One, machapisho na vipeperushi, pamoja na CDs. Elimu kwa waandishi 170 ilitolewa kuhusu masuala ya fedha na uchumi.

Wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki

Hadi kufikia tarehe 30/11/2008 wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki 31,444 wamelipwa mafao yao kwa mujibu wa Hati ya Makubaliano. Aidha, Hazina bado inapokea na kuyafanyia kazi madai ya mstaafu mmoja mmoja na yanapothibitika kuwa yanastahili kulipwa yanalipwa.

5.6 KUIMARISHA MASHIRIKA YA UMMA/UBINAFSISHAJI

Ilani ya Uchaguzi ya CCM, imeelekeza yafuatayo:

(i) Kuendelea na ubinafsishaji na ukodishaji wa viwanda na mashirika ya umma yaliyobaki. Ili kufikia malengo hayo ya jumla hatua zitachukuliwa kuvutia wawekezaji katika ufufuaji wa viwanda vilivyopo na kujenga vipya katika sekta zilizopewa kipaumbele.

(ii) Kutafuta wabia wa kuendeleza miundombinu ya kiufundi iliyopo nchini yenye uwezo wa kutengeneza mashine na mitambo na kukuza uwezo wa kutengeneza vipuri mbalimbali.

Utekelezaji

Ili kufanikisha haya, Wizara ya Fedha na Uchumi, imeendelea kusimamia ubinafsishaji wa mashirika ya umma kupitia Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) hadi Deseaba 2007 ilipomaliza muda wake na majukumu yake kuhamishiwa Consolidated Holdings Company (CHC). Aidha, chini ya Sheria ya Bunge Namba 10 ya mwaka 2007 pia CHC ilikabidhiwa majukumu ya kusimamia na kuendeleza kazi zilizokuwa za Loans and Advances Realization Trust (LART) na Air Tanzania Holding Company (ATHCO). Kazi hizi ni pamoja na mashirika 28 yaliyokuwa kwenye ufilisi yenye jumla ya shilingi bilioni 6.5 na mashauri 25 yaliyokuwa Mahakamani, yote hayo yakihusu LART; na mashauri 15 yaliyohusu ATHCO. Chini ya mabadiliko mengine yaliyoletwa na sheria ya *The National Bank of Commerce (Reorganisation and*

Vesting of Assets and Liabilities) (Amendment)(No.2)Act,2007, CHC ilikabidhiwa dhamana ya kusimamia na kuendeleza kazi zilizokuwa zinafanywa na Simu 2000 Ltd. Kazi zilijumuisha mashirika 37 yaliyokuwa chini ya ubinafsishaji; madeni yapatayo shilingi bilioni 7.9 pamoja na madai mbalimbali yapatayo sh. bilioni 7.2. Sheria hii pia iliongeza uhai wa CHC kwa miaka minne hadi Juni 2011. Kwa mwaka ulioshia Desemba 2007 CHC iliweza kupata mapato ya shilingi bilioni 8.0 na matumizi yakiwa shilingi bilioni 4.7 na hivyo kupata ziada ya shilingi bilioni 3.3.

Ubinafsishaji wa mashirika ya umma

Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2007 jumla ya mashirika 336 na mali mbalimbali zipatazo 666 (non-core assets) yalikuwa yamebinafsishwa na iliyokuwa Tume ya Rais ya kurekebisha Mashirika ya Umma. Zoezi zima la ubinafsishaji limejumuisha mikakati mbalimbali zilizotumika kama vile upangishaji, uuzaji wa mali, ubia na ukodishaji. Ubinafsishaji umeleta mafanikio yafuatayo:

(i) Mashirika yaliyobinafsishwa na kuanza kufanya kazi sasa yanalipa kodi Serikalini badala ya kutegemea ruzuku;

(ii) Wawekezaji kutoka nje wameongezeka kwa kuwekeza katika mashirika yaliyobinafsishwa;

(iii) Uzalishaji katika baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa umeongezeka maradufu;

(iv) Ajira zimepatikana pale ambapo haikuwepo kwa yale mashirika yaliyokuwa yamefungwa;

(v) Ajira zimeboreshwa kwa kuwa na malipo mazuri zaidi;

(vi) Teknolojia katika mashirika mengi ilikuwa ya kale, lakini sasa teknolojia mpya imepatikana na hivyo kupata ubora wa bidhaa; na

(vii) Watanzania wamewezeshwa, ambapo wengine wamepata fursa ya kununua hisa na kuwa wamiliki wa mashirika yaliyobinafsishwa.

Programu ya ubinafsishaji inaendelea ambapo mashirika 34 yako katika hatua mbalimbali, ikiwemo uuzaji wa hisa za Serikali kwa wawekezaji binafsi na ufuatiliaji wa mashirika yaliyokwishabinafsishwa.

6.0 HITIMISHO

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Wizara ya Fedha na Uchumi ilijizatiti kutekeleza malengo yaliyo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Matokeo ya utekelezaji huo, ni kwamba kumekuwepo na mafanikio makubwa katika maeneo mengi yanayosimamiwa na Wizara. Uchumi umeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka na kufikia asilimia 7.1 mwaka 2007 ukilinganisha na asilimia 6.7 mwaka 2006.

Bajeti ya Serikali imeongezeka kutoka shilingi trilioni 4.18 mwaka 2005/06 hadi shilingi trilioni 7.22 katika mwaka 2008/09 sawa na ongezeko la asilimia 72.8. Makusanyo ya mapato ya ndani yamefikia zaidi ya wastani wa shilingi bilioni 300 kwa mwezi ikilinganishwa na shilingi bilioni 150 kwa mwezi mwaka 2005/06; mfumuko wa bei umekua kwa kiwango cha chini hadi Juni 2008; miundombinu hasa ya barabara na mawasiliano imeboreka; sekta za elimu na afya zimeendelea kupanuka; kilimo kinakua kwa wastani wa asilimia 4 kwa mwaka; na Pato la kila Mtanzania linaendelea kuongezeka kutoka shilingi 441,030 mwaka 2005 hadi shilingi 546,956 kwa takwimu za mwaka 2007.

Sheria za kodi na za uwekezaji zimeendelea kuvutia wawekezaji nchini. Aidha, uamuzi wa Serikali wa kuacha kukopa kutoka benki za ndani kumewezesha mikopo kwa sekta binafsi kuongezeka. Ufanisi na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa ujumla umeongezeka kutokana na kuboreshwa kwa Sheria ya Fedha na ya Manunuzi ya Umma.

NA MSEMAJI MKUU - WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI
DESEMBA 2008